# HALMASHAURI YA MJI GEITA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA UGAVI NA MANUNUZI TAREHE 29/10/2021-KIKAO MAALUM.**

**MAHUDHURIO** **WADHIFA**

1. LEONARD CHACHA ........................ MWENYEKITI
2. PATRICK R. NDABA ..........................KATIBU
3. DR. CLEMENCE KONKAMKULA .........MJUMBE
4. THECLA GASEMBE........................... MJUMBE
5. ROBERT MATUNGWA .......................MWANASHERIA

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

1. MARGARETH MACHA.........................KWA TAARIFA
2. PIUS F.MAGOTI..................................KWA TAARIFA

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE WAKARIBISHWA**

1. ENG. OSWALD MTEI......................... MHANDISI UJENZI
2. RASHID MUHAYA..............................AFISA ELIMU SEKONDARI

**SECRETARIETI**

1. METHOD LILY .................................AFISA UGAVI MSAIDIZI
2. ELLY OMEME...................................AFISA UGAVI MSAIDIZI

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za kikao
3. Kupitisha njia za manunuzi katika miradi ya ujenzi kwa fedha za UVIKO-19
4. Kupitisha Njia za Manunuzi na kupitisha nukuu za bei za vifaa mbalimbali vinavyotakiwa kununuliwa/kutengenezwa kwa mawakala na Wazbuni.
5. Kufunga kikao.

**AGENDA NAMBA 1: 29/10/2021 : KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti wa bodi ya zabuni alifungua kikao mnamo saa 4:30 asubuhi kwa kuwasalimu wajumbe na kuwaomba kutoa ushirikiano wa mawazo na ushauri katika kikao hicho.

**AGENDA NAMBA 2: 29/10/2021: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKA**



Scanned with CamScanner

Mwenyekiti alimkaribisha katibu ili aweze kuwasomea wajumbe ajenda zinazotegemewa kujadiliwa katika kikao hicho ambapo jumla ya ajenga nne zilisomwa na wajumbe waliridhia ajenda hizo zote zilizowasilishwa na katibu wa bodi ya zabuni.

**AGENDA NAMBA 3: 29/10/2021 : KUPITISHA NJIA ZA MANUNUZI KATIKA MIRADI YA UJENZI KWA FEDHA ZA UVIKO-19**

Katibu wa Bodi ya zabuni aliwaeleza wajumbe kwamba Idara za Elimu Msingi na Sekondari zimewasilisha dokezo la kuomba kuendelea na taratibu za manunuzi kwa fedha zilizotolewa na Serikali kwa ujenzi wa miundombinu ya madarasa 61 katika shule za sekondari na madarasa mawili (2) ya shule shikizi za msingi ikiwa zimetolewa jumla ya Tshs.illioni moja na million mia mbili na sitini (1,260,000,000.00).

Kitengo cha Ugavi na Manunuzi na Ugavi kilipendekeza njia zitakazotumika kwa mujibu wa Kanuni/miongozo viliyotolewa ziwe ni zile za manunuzi ya kutumia Force Account,Ununuzi wa Pamoja (Bulk Procurement) na Ununuzi wa kutumia watengenezaji wa moja kwa moja viwandani (Procurement from Manufacturer/Factory) na kutumia Mawakala au Wazabuni.

**Wajumbe wa bodi ya zabuni waliridhia kwamba njia zitakazotumika kufanya manunuzi katika miradi ya UVIKO-19 ni kwa kutumia Force Account,Ununuzi wa Pamoja (Bulk Procurement) na Ununuzi wa kutumia watengenezaji wa moja kwa moja viwandani (Procurement from Manufacturer/Factory) na kutumia Mawakala au Wazabuni.**

**AGENDA NAMBA 4: 29/10/2021 KUPITIA NUKUU ZA BEI ZA UNUNUZI WA VIFAA MBALIMBALI VINAVYONUNULIWA KWA MAWAKALA/WAZABUNI NA WATOA HUDUMA WENGINE KWA FEDHA ZA UVIKO-19**

Mwenyekiti alimkaribisha katibu ili aweze kuwasilisha agenda hiyo ndipo katibu akawasomea wajumbe nukuu za bei za vifaa mbali mbali katika mchanganuo ufuatao :-

A. ZABUNI YA KUTENGENEZA FREMU NA TOP ZA MILANGO YA MITI MIGUMU KWA AJILI YA MADARASA YANAYOJENGWA KWA MRADI WA UVIKO 19

Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kilitembeza nukuu za bei za utengenezaji wa top za milango kwa ajili ya madarasa 63 ambapo jumla ya wazabuni watatu waliweza kujaza gharama zao katika mchanganuo ufuatao :-

a) M/S Amos Charles Magusu S.L.P aliomba kwa Tshs.22,680,000.00 sawa na 360,000/=@ Mlango uliokamili.
b) M/S Mando Women Group S.L.P aliomba kwa Tshs.33,453,000.00 sawa na 531,000/=@ Mlango uliokamili.
c) M/S Ibrahim Ngaye S.L.P aliomba kwa Tshs.107,000,000/- sawa na 1,698,000/=@ Mlango uliokamili.



Scanned with CamScanner

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa, Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kimempendekeza mzabuni M/S Amos Charles Magusu kwa kuwa gharama zake zipo chini na Kitengo kimeleta bodi ya zabuni ili kupata idhini.
Wajumbe wa bodi ya zabuni waliridhia mzabuni Amos Charles Magusu apewe kazi ya utengenezaji wa fremu na top za milango kwa jumla ya shilingi 22,680,000.00 kwa fremu na top 63 ambapo kila fremu na top itagharimu shilingi 360,000.00

B. ZABUNI YA UNUNUZI WA VITI NA MEZA KUPITIA FEDHA ZA MRADI YA UVIKO 19

Katibu aliwajulisha wajumbe wa bodi kuwa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kilitembeza nukuu za bei za utengenezaji wa viti na meza seti 3050 za Shule za Sekondari na Madawati 50 kwa ajili ya madarasa mawili ya shule Shikizi ya Msingi, ambapo jumla ya wazabuni watatu waliweza kujaza gharama zao katika mchanganuo ufuatao:-

a) M/S Reuben Bigora S.L.P aliomba kwa Tshs.232,500,000/= sawa na Tshs.75,000 kwa seti kwa Shule za Sekondari na dawati moja la Shule Shikizi ya Msingi.

b) M/S Mando Women Group aliomba kwa Tshs.256,000,000/= sawa na Tshs.82,580 kwa seti kwa Shule za Sekondari na dawati moja la Shule Shikizi ya Msingi.

c) M/S Maemba Malegesi Kigwa aliomba kwa Tshs.226,300,000/= sawa na Tshs.73,000 kwa seti kwa Shule za Sekondari na dawati moja la Shule Shikizi ya Msingi.

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa, Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kimempendekeza mzabuni M/S Maemba Malegesi Kigwa kwa kuwa gharama zake zipo chini na Kitengo kimeleta bodi ya zabuni ili kupata idhini.

C. ZABUNI YA UTENGENEZAJI NA UFUNGAJI WA MADIRISHA YA ALLUMINIUM

Katibu aliwasilisha agenda hiyo kwa kuwasomea wajumbe orodha ya wazabuni waliojaza nukuu za bei katika zabuni hiyo kwa mchanganuo ufuatao :-

| NA. | JINA LA MZABUNI | GHARAMA /KIASI |
|---|---|---|
| 1. | ARFA GLASS AND GENERAL SUPPLY, S.L.P 265 GEITA | 88,200,000.00 |
| 2. | MAIGE MAGANDULA JAPHET, S.L.P 11 GEITA | 94,500,000.00 |
| 3. | MANDO WOMEN GROUP , S.L.P 167 GEITA | 110,250,000.00 |

Baada ya mapitio hayo ya nukuu ya bei za wazabuni wa utengenezaji wa madirisha ya alluminium katika shule za sekondari na msingi, wajumbe wa bodi ya zabuni walimpitisha mzabuni M/S ARFA GLASS AND GENERAL SUPPLY kwa gharama ya shilingi 88,200,000.00 ikiwa kila dirisha litagharimu kiasi cha shilingi 280,000.00.



Scanned with CamScanner

**Wajumbe wa bodi ya zabuni waliridhia mzabuni Maemba Malegesi Kigwa apewe kazi ya utengenezaji wa viti na meza kwa jumla ya shilingi 226,300,000.00 kwa fremu na top 63 ambapo kila fremu na top itagharimu shilingi 360,000.00**

D. ZABUNI YA UNUNUZI WA VIFAA VYA VIWANDANI KWA KUTUMIA WAKALA/MZABUNI KUPITIA FEDHA ZA MRADI WA UVIKO 19

Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kilitembeza nukuu za bei za vifaa vya viwandani ambapo jumla ya wazabuni waliweza kujaza gharama zao katika mchanganuo ufuatao :-

| NA. | JINA LA MZABUNI | GHARAMA /KIASI |
|---|---|---|
| 1. | M/S OTONDE HARDWARE | 680,638,600.00 |
| 2. | M/S CLASK TANZANIA LIMITED | 926,753,120.00 |
| 3. | M/S ROMORE SUPPLY AND CONTRACTORS | 918,772,000.00 |

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa, katika wazabuni hao watatu , mzabuni mmoja hakuweza kukamilisha ujazaji wa gharama ambaye ni M/S Mara General Supply lakini wazabuni wawili waliweza kukamilisha kujaza nukuu hizo za bei. Pia katibu aliwaeleza wajumbe kuwa baada ya wazabuni kuwasilisha gharama zao Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kilienda sokoni kujiridhisha kama bei za wazabuni hao zinaendana na soko na kukubaliana kumpitisha mzabuni M/S Otonde Hardware kwa gharama ya shilingi 680,638,600.00 kwa vifaa vyote kwa kuwa gharama zake zilikuwa chini na zinaendana na bei ya soko.

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Kitengo cha Ugavi kimeleta swala hili bodi ya zabuni ili kupata idhini kabla ya kuingia mkataba na mzabuni huyo,

**Wajumbe wa bodi ya zabuni waliridhia mzabuni M/S Otonde Hardware apewe kazi ya usambazaji wa vifaa vya viwandani kwa jumla ya shilingi 680,638,600.00 lakini wakasisitiza gharama za mzabuni huyo ziwe zimeendana na soko.**

**AGENDA NAMBA 4: 29/10/2021 : KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa ushiriki wao mzuri katika kikao hicho na alisisitiza ufuatiliaji wa posho za vikao vya bodi ya zabuni kufanyika ili wajumbe waweze kupata stahiki zao na pia akasisitiza ufanyike utaratibu wa kuwawezesha wajumbe kwenda mafunzo ya Sheria na maswala ya kimanunuzi ili wawe na uelewa pindi wanapofanya maamuzi. Baada ya kusema hayo mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 5: 48 asubuhi.

**UMETHIBITISHWA :**

| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
|---|---|
| Jina Leonard Chacha | Jina PATRICK RINDABA |
| Sahihi [signature] | Sahihi [signature] |
| Tarehe 11/11/2021 | Tarehe 11/11/2021 |



Scanned with CamScanner